



APPEL DE GENÈVE
GENEVA CALL

**Kupiga marufuku mabomu
ya kutegwa ardhini kwa nia ya
kujeruhi: Kanuni kuu kutoka
Hati ya Ahadi ya shirika la
Geneva Call**



APPEL DE GENÈVE
GENEVA CALL

info@genevacall.org
www.genevacall.org





1

Usitumie mabomu ya kutegwa

ardhini katika hali yoyote ile



2

Usitengeze mabomu ya kutegwa ardhini



3

Kamwe usipeleke, au kupokea, kununua, ya kutegwa ardhini. Mabomu yote ya

kutoa, kushiriki biashara au kuuza mabomu kutegwa ardhini sharti yaangamizwe



4

Usichunge mabomu
ya kutegwa ardhini



Mabomu ya kutegwa zote
zinapachwa kubomolewa



5

Fanya kila uwezalo kuzuia mtu yeyote kwa nia ya kujeruhi kupitia eneo lako,

kusafirisha mabomu ya kutegwa ardhini au kutumia mabomu hayo katika eneo lako



6

Weka alama, unakili na kupiga ripoti yote unayojua au unayoamini

kwa mkubwa wako kuhusu maeneo kuna mabomu yaliyotegwa



7

Watahadharishe raia na jamii, hususa kutegwa ardhini na kuwashauri wakae

watoto, kuhusu hatari za mabomu ya mbali na maeneo yenye mabomu



8

Toa ushirikiano katika shughuli ya kuondoa mabomu ya kutegwa ardhini



9

Wasaidie waathirika wa mabomu ya ukikumbuka kwamba nao wanastahili

kutegwa ardhini kadiri ya uwezo wako, kuheshimiwa na kuhurumiwa



10

Himiza na kutoa maelezo kuhusu
ya kutegwa ardhini kwa watu

umuhimu wa kupigwa marufuku mabomu
unaokutana nao-wapiganaji na raia



11

Zingatia

kanuni hizi



12

Vitendo vya kukiuka sheria lazima viadhibiwe kwa mujibu wa viwango vya kimataifa



13

Shirikiana na shirika la Geneva Call kufuatilia

na kuhakikisha kanuni hizi zinaheshimiwa



APPEL DE GENÈVE
GENEVA CALL

Geneva Call

Geneva Call ni shirika lisilo la kiserikali, lisiloegemea upande wowote, na ambalo hujihusisha katika kufanya mashauriano na makundi yenye silaha yasiyotoka serikalini, katika kuhimiza kuzingatiwa na kuheshimiwa kwa kanuni za kimataifa kuhusu utoaji wa misaada ya kibinadamu.

Shirika la Geneva Call linaelekeza utendaji wake kwenye ulinzi wa raia walio kwenye mazingira ya vita, na hususan:

- Usalama wa watoto
- Kuzuia unyanyasaji wa kimapenzi na kuondoa ubaguzi wa kijinsia
- Kupigwa marufuku mabomu ya kutegwa ardhini kwa nia ya kujeruhi

Hati ya Ahadi

Hati ya Ahadi ni nyaraka rasmi zinazotwa sahihihi na wadau katika mizozo, ambao hawatoki serikalini, wakiahidi kuheshimu kanuni za kimataifa za utoaji msaada wa kibinadamu.

Hadi kufikia sasa, shirika la Geneva Call limeandaa aina tatu za nyaraka hizo:

- *Hati ya kuahidi* kuzingatia kupigwa marufuku mabomu ya kutegwa ardhini kwa nia ya kujeruhi, na kutoa ushirikiano katika juhudi za kutegua mabomu kama hayo
- *Hati ya kuahidi* Kuwalinda Watoto kutokana na athari za mapigano
- *Hati ya kuahidi* kuzingatia kupigwa marufuku unyanyasaji wa kimapenzi kwenye mazingira ya vita na kuondolea mbali ubaguzi wa kijinsia

Shirika la Geneva Call huunga mkono na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa hizo Hati za Ahadi na makundi yenye silaha, yasiyo ya serikali, yaliyotia sahihi.

Marufuku dhidi ya mabomu ya kujeruhi

Marufuku dhidi ya mabomu ya kutegwa ardhini kwa nia ya kujeruhi inatakiwa kueleweka kuwa ni kupigwa marufuku kabisa kwa mabomu yanayodhamiriwa kuwalipukia waathirika, na ambayo hulipuka kutokana na kuwepo, kuwepo karibu na, au kugusa mtu; mkiwemo mabomu mengine yanayowalipukia waathirika au magari na kusababisha athari sawa na hizo, yawe ya kutengenezwa kiwandani au ya kujitengenezea.